# *Hijaab*

*Lulu Iliyohifadhika*



Himdi Zote Anastahiki Allaah Aliyetukuka Mola wa walimwengu wote, Swalah na salamu zimshukie kipenzi chetu Mtume Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na Swahaba zake (Radhiya Allaahu 'anhum) na watangu wema mpaka Siku ya Mwisho.

Anasema Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala): ((Na waambie Waumini wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasidhihirishe mapambo yao [na viungo vyao] isipokuwa vinavyodhihirika. Na waangushe shungi zao mpaka vifuani mwao, na wasionyeshe mapambo yao ila kwa waume zao, au baba zao, au baba wa waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au kaka zao, au wana wa kaka zao, au wana wa dada zao, au wanawake wenzao, au iliyo wamiliki mikono yao ya kuume, au wafuasi wanaume wasio na matamanio, au watoto ambao hawajajua mambo yaliyohusu uke. Wala wasipige miguu yao ili yajulikane mapambo waliyoyaficha. Na tubieni nyote kwa Allaahh enyi Waumini, ili mpate kufaulu)) [An-Nuwr 24: 31]

Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) Aliposema wanawake wavae Khimaar, Hakumaanisha kuwa wavae leso kubwa tu, bali ni kuwa mwanamke akivaa hiyo Khimaar, itamfunika mapambo yake muhimu, nayo ni masikio, shingo na kifua. Kwa hivyo, mwanamke akivaa kitambaa kidogo ambacho hakimsitiri mapambo yake hayo tuloyataja, basi hiyo si Hijaab

Baada ya kuona katika Qur-aan kuwa Hijaab ni waajib, inampasa mume kumhimiza mkewe na kumshawishi avae Hijaab ili aheshimiwe na athaminiwe kuwa ni mcha Mungu. Katika Aayah nyengine Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) Anawahutubia wanawake wa Kiislamu wasioneshe mapambo yao kama walivyokuwa wakifanya wanawake wakati wa jaahiliyyah (kabla Uislamu). Wanawake wa jaahiliyyah walikuwa wakivaa nguo ndefu lakini mapambo yao kama vile shingo, masikio, nywele na kadhalika yote yalikuwa yakionekana.

Vilevile, Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) Anasema: ((Ee Mtume! Waambie wake zako, na binti zako, na wanawake wa Kiislamu [wengine] wajiteremshie uzuri nguo zao. Kufanya hivyo kutapeleka upesi wajulikane [kuwa ni watu wa heshima] wasiudhiwe. Na Allaah ni *Ghafuwrar-Rahiymaa* [Mwingi Wa Kughufiria - Mwenye Kurehemu)) [Al-Ahzaab 33: 59].

Aayah hii Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) Anamwambia Mtume (Swalla Allaahu 'alahyi wa aalihi wa sallam) awaamrishe: (i) wake zake (ii) binti zake (iii) Waumini wanawake. Wajifunike ili wajulikane kuwa ni watu wa

heshima wasipate kuudhiwa. Ilipoteremka Aayah hii, Maswahaabiyyaat katika mji wa Madiynah walitoka wakiwa wamejifunika mwili mzima gubigubi na kubakisha jicho moja tu la kutazamia. Hii ni dalili mojawapo ya Wanavyuoni kuthibitishia kwamba Niqaab ni waajib kwa Mwanamke wa Kiislamu.

Aayah za Hijaab zlipoteremka tu, wanawake wote walitoka huku wamejifunika kama ilivyoamrishwa. Waume zao waliposikia Aayah hizo, waliwaeleza wanawake maana yake, basi wanawake walikuwa tayari Kufuata shari'ah ya Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) kama Alivyoamrisha katika Qur-aan. Madhali walikuwa hawana uwezo wa kununua nguo mpya, walinyanyua nguo zao kwa sehemu mbili ili watumie kama Hijaab. Hiyo ni kinyume na vile wanawake wa kisasa walivyo. Wao hutoa visingizio kwa kutovaa Hijaab inayotakikana.

**Sharti Za Hijaab (Vazi la mwanamke)**

1- Ifunike mwili mzima isipokuwa ilivyotajwa (uso na viganja, na Wanavyuoni wengine wanaona mpaka uso).
2- Nguo zisiwe na mapambo (hata 'abayah haipasi kuwa na marembo).
3- Iwe nzito isiyoonyesha ndani. Mtume (Swalla Allaahu alayhi wa aalihi wa sallam) amesema: *((Aina mbili za watu wa motoni siwaoni... Wanawake ambao wamevaa lakini wako uchi, wanawashawishi wanaume wawatongoze, na wanaelekea kwao [kwa kuwa warahisi]. Vichwa vyao kama nundu za ngamia zinazoyumba [aina ya msuko wa nywele wanaosuka wanawake]. Hawatoingia Peponi wala hawatosikia harufu yake ingawa harufu yake inaweza kunuswa kutoka masafa kadhaa na kadhaa)).* [Muslim]
4- Isibane mwili ukaonekana muundo wa mwili, bali iwe pana kabisa. Mtume (Swalla Allaahu 'aalyhi wa aalihi wa sallam) amesema: ((Kikundi cha wanawake hawatoingia peponi. Hao ni miongoni mwa wale wanaovaa nguo za kubana, za kuonyesha mwili na hawafuati amri ya Allaah ya kuvaa Hijaab. Hawatoingia tu Peponi bali hata hawatosikia harufu ya Pepo ambayo harufu yake husikilizana masafa ya mwendo wa miaka 500)). [Imesimuliwa na Muslim]
5- Isitiwe manukato wala mwanamke asijitie manukato. Abu Muwsaa Al-Ash-'ariy (Radhiya Allaahu 'anhu) amesema kwamba, amesema Mjumbe wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema: *((Mwanamke yeyote yule atakayejitia manukato akapita mbele ya watu ili waipate harufu yake basi huyo ni mzinifu* [atakuwa amezini])) [Imepokewa na Ahmad katika musnad yake.
6- Isiifanane na mavazi ya kiume. Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anhu) amesema: "Mjumbe wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amemlaani mwanamme mwenye kuvaa mavazi ya mwanamke na mwanamke mwenye kuvaa mavazi ya mwanamme." [Imepokelewa na Abu Daawuwd],

7- Isifanane na mavazi ya makafiri.

8- Isiwe nguo ya fakhari kwa kutaka kujionyesha.

Tunamuomba Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) Awawezeshe dada zetu kufuata amri Zake na za Mjumbe Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) ili wapate Radhi Zake na Awalipe mema duniani na Aakhirah.  Aamiyn.



**Tafadhali chapisha idadi zozote uwezazo na uzigawe kwa dada zetu wa Kiislamu.**

**www.alhidaaya.com**